Toleo 64 - Ramadhan 1443 AH / Mei 2022 M

# UQAB
Jarida la


**TAARIFA KWA VYOMBO VYYA HARABI**
Tangazo la Natija ya Kuutafuta Mwandamo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhan wa Mwaka 1443 Hijri

**HABARI NA MAONI**
Kipimo cha Sarafu ya Dola ndio Chanzo cha Mfumuko wa Bei

**TOLEO JIPYA**
Bangladesh Yazifunga Shule za Waislamu wa Rohingya

**JIBU LA SWALI**
Matarajio ya Wakoloni Nchini Tanzania

# Tunapongeza Umma wa Kiislamu kuingia Mwezi Mtukufu wa Ramadhan



Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir Kenya

بسم الله الرحمن الرحيم

﴿وعد الله الذين آمنوا منكم وعملوا الصالحات ليستخلفنهم في الأرض كما استخلف الذين من قبلهم وليمكنن لهم دينهم الذي ارتضى لهم وليبدلنهم من بعد خوفهم أمنا يعبدونني لا يشركون بي شيئا ومن كفر بعد ذلك فأولئك هم الفاسقون﴾

KUMB: 09/1443 Jumanne, 26 Shaaban 1443 H 29/03/2022 M

**Taarifa kwa Vyombo Vya Habari**

# Tunapongeza Umma wa Kiislamu kuingia Mwezi Mtukufu wa Ramadhan

Hizb ut- Tahrir Kenya kwa furaha inatuma salamu za pongezi kwa Waislamu nchini na kote ulimwenguni kwa ujumla kuingia mwezi mtukufu wa Ramadhan. Tunapoingia kwenye mwezi huu wa Rahma, Msamaha na kuachwa huru na moto, tunamuomba MwenyeziMungu (swt) atupe nguvu na afya za kutelekeza ibada tukufu ya swaum ambayo sio faradhi tu bali pia ni mojawapo ya nguzo tano za Uislamu.

Mwenyezi Mungu Subhaanahu wa Ta’ala ameufanya uchaMungu kuwa ndio lengo hasa katika ibada hii tukufu. Uchamungu ndio msingi wa utambulisho wa Kiislamu unaopaswa kudhihirika na kuonekanwa katika matendo yote ya waumini katika kutekeleza maamrisho ya Mwenyezi Mungu na makatazo yake. Na ili jamii nzima iweze kuwa na uchaji Mungu kunahitajika dola inayowajibika katika kutekeleza Uislamu katika nyanja zote za maisha. Tunaeleza bayana kwamba dola hii sio nyengine bali ni Khilafah ambayo kwa idhini ya Mwenyezi Mungu itasimamishwa katika mojawapo ya nchi za Kiislamu.

Jamii ya Kiislamu inapoingia katika mwezi huu uliobarikiwa, bei za bidhaa muhimu kama vile mafuta ya kupikia, mafuta, unga wa ngano, sukari ni ghali sana. Huku wananchi wakiendelea kuteseka na wengine kufariki kutokana na njaa kali katika baadhi ya maeneo nchini, wanasiasa wa mirengo yote ya kisiasa wamejikita katika kampeni za domo kaya kujitafutia vyeo huku wakiwaahidi Wakenya maskini ahadi tupu! Hili linafaa kuwa ukumbusho tosha kwa jamii ya Kenya kwamba uongozi wa kibepari haujali maslahi ya raia wake.

Ingawa vita vya Ukraine vimeathiri uchumi wa dunia kwa kiasi fulani kwa kuzingatia hali ya soko ya bei ya mafuta duniani kwani vita hivi vinazunguka mataifa yanayoongoza, hii hata hivyo, sio sababu kuu kabisa ya mfumko wa bei wa sasa wa kimataifa. Mfumo wa uchumi wa kibepari umefanya bei kuwa msingi wa uzalishaji na usambazaji wa mali. Zaidi ya hayo, Mfumo hutumia sera ya fedha za makaratasi bila thamani ya ndani katika sarafu yake kuifanya iwe ya kupunguka kwa bei kila mara.

Twamoumba Mwenyezi Mungu SWT atakabali amali zetu na kuupa Umma huu mlinzi na kinga halisi nayo ni Khilafah kwa mfumo wa Utume. Khilafah ndio kwa mara nyengine tena itawanasua wanadamu kutoka majanga haya ya Kiuchumi.

**Shabani Mwalimu**

**Mwakilishi kwa Vyombo Vya Habari Hizb ut-Tahrir Kenya**

Afisi kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir

بسم الله الرحمن الرحيم

﴿وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ﴾

KUMB: 28/1443 | Ijumaa, 29 Shaaban 1443 H | 01/04/2022 M


**Taarifa kwa Vyombo Vya Habari**

# Tangazo la Natija ya Kuutafuta Mwandamo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhan wa Mwaka 1443 Hijri

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwingi Kurehemu, na sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa walimwengu wote, aliyeteremsha Qur'an na akatuchagulia Uislamu kuwa ndio Dini yetu, na rehma na amani zimshukie yule aliye anzisha Umma wa Kiislamu, bwana wa viumbe, bwana wetu Muhammad na juu ya familia yake na maswahaba zake wote.

Imepokewa kutoka kwa Bukhari katika Sahih yake kutoka kwa Muhammad bin Ziyad kwamba amesema: “Nilimsikia Abu Hurairah (radhi za Allah ziwe juu yake) akisema: Amesema Mtume (saw) au amesema Abu Al-Qasim (saw): «صُومُوا لِرُؤْيَتِهِ وَأَفْطِرُوا لِرُؤْيَتِهِ فَإِنْ غُبِّيَ عَلَيْكُمْ فَأَكْمِلُوا عِدَّةَ شَعْبَانَ ثَلَاثِينَ» **"Fungeni kwa kuonekana kwake (mwandamo wa mwezi wa Ramadhan), na fungueni kwa kuonekana kwake (mwandamo wa mwezi wa Shawwal), ni ikiwa mawingu yatawaziba (kutouona mwezi), basi kamilisheni idadi ya siku thalathini za Sha'aban."**

**Baada ya kuutafuta mwandamo wa mwezi wa Ramadhan iliyobarikiwa usiku huu, mkesha wa kuamkia Jumamosi, kuonekana kwa mwezi mwandamo kumethubutu kulingana na masharti ya muandamo wa Kishariah, katika baadhi ya nchi za Waislamu, kwa hiyo kesho, Jumamosi, ni siku ya kwanza ya mwezi mtukufu wa Ramadhan wa mwaka 1443 Hijria.**

Kwa mnasaba huu, nafikisha salamu na pongezi zangu za Mkuu wa Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na wote wanaofanya kazi ndani yake, kwa Amiri wa Hizb ut Tahrir, mwanachuoni mkubwa, Ata Bin Khalil Abu Al-Rashtah, nikimuomba Mwenyezi Mungu amsaidie na aharakishe ushindi kwetu na tamkini kupitia mikono yake.

Ramadhan mwaka huu inakuja katika wakati ambapo nchi za Magharibi zinajaribu kugeuza mashambulizi yake ya kimaadili, ambayo zimeyaendesha katika karne nzima ya maisha ya kibinafsi ya Waislamu, kuwa mashambulizi ya moja kwa moja dhidi yake. Baada ya kushindwa kwa kampeni ya "vita dhidi ya ugaidi" kuunda roho ya kusalimu amri katika Umma wa Kiislamu, na baada ya mshtuko wa mapinduzi ya Kiarabu ambayo watawala wa Magharibi walisibiwa nayo, yaliyogeuza meza dhidi ya vibaraka wao na kukaribia kuufukuza ushawishi wa Magharibi nje ya ardhi yetu, kwa kiwango ambacho mkuu wao alisema kwamba yalikigeuza kichwa chake kuwa na mvi! Baada ya mishtuko hii Magharibi ilitambua kwamba maumbile ya Uislamu na Waislamu yanaamuru kwamba kasi ya uasi wa Waislamu dhidi ya hali ya kikoloni itaongezeka mfululizo, na itaendelea kuongezeka hadi Waislamu pasi na budi waregeshe tena mamlaka yao.

Lakini suala la kutia shinikizo dhidi ya Urusi na kuzingirwa kwa China limekuwa suala la dharura kwa maslahi ya Magharibi inayoongozwa na Marekani. Hili lilihitaji kuondolewa kwa sehemu kubwa za vikosi vya kijeshi na vifaa vya Magharibi kutoka kwa nchi za Kiislamu. Lakini Magharibi haitaki kuuacha Umma wa Kiislamu upate pumzi yake wasije wakarudia tena vile vitendo dhidi ya vibaraka wao. Kwa ajili hiyo, wakaanza kuchukua hatua za kuwashughulisha Waislamu wenyewe kwa wenyewe, kwa kuyachezea maisha yao ya kibinafsi kote duniani; na kwa hili, wakahamasisha vibaraka na zana zote kuyabadilisha hadi watakaporegea. Walizidisha maradufu usawazishaji mahusiano kati ya watawala katika nchi za Waislamu na umbile la Kiyahudi, na wakaingiza makundi ya Mayahudi kwenye dola za Ghuba ya Kiarabu, na wakaanza kuishambulia ghariza ya dini katika ardhi ya Misikiti Miwili Mitakatifu. Wakawafunga wanachuoni na wakaibadilisha Kamati ya Kuamrisha Mema kwa Kamati ya Burudani iliyozingira Al-Madina Al-Munawwarah na Makka Al-Mukarramah kwa machafu na maovu.

Aya za Qur’an ziliondolewa kwenye mitaala ya elimu nchini Jordan, wakaanzisha jambo hilo hilo katika mitaala ya Misri, na wakaingiza mitaala ya elimu hiyo katika maeneo yaliyokombolewa nchini Syria. Watawala wa Nyumba ya Saud waliondoa katika mitaala ya elimu yale ambayo Mwenyezi Mungu (swt) alikuwa amewalaani Mayahudi kwayo. Mtawala wa Misri alianza kufufua ustaarabu wa kifirauni katika sherehe ya kimataifa ya miili ya mafirauni wa kifalme. Amerika iliwaachilia Mabaniani wenye chuki kuwatesa Waislamu katika Bara dogo la India, hivyo wakaichuna

*Endelea... UK 4*

Kashmir na kuwafukuza Waislamu kutoka Assam na kuwanyima haki za kiraia idadi kubwa ya Waislamu nchini India, na kuanza kuwazuia wanawake wa Kiislamu kuvaa Khimar (hijab) kupitia nguvu ya idara ya mahakama na sheria.

Vile vile barani Ulaya, Ufaransa iliishambulia jamii yake ya Kiislamu, hivyo ilianza kwa kufunga misikiti na kutunga sheria za kuingilia jinsi Waislamu wanavyowalea watoto wao ndani ya nyumba zao. Ama nchi za Skandinavia zikiongozwa na Sweden zilizidisha mashambulizi dhidi ya familia za Kiislamu na kuanza kuwachukua watoto wa Kiislamu na kuwaficha kutoka kwa familia zao kwa visingizio vya uongo. Hili liliambatana, katika nchi za Kiislamu, na kuanza kwa mchakato wa kuanzisha vifungu vya CEDAW vya kuisambaratisha familia ya Kiislamu, hasa katika Ardhi Iliyobarikiwa ya Palestina kwa kuharamisha ulezi wa baba juu ya familia yake na kuifanya familia na mkuu wa familia kuwa chini ya huruma ya wasio na maadili. Hatusahau madhihirisho ya kuwapokea wauaji wa Waislamu na wanyakuzi wa ardhi yao na heshima yao katika wiki za hivi karibuni; dhihirisho la kujifanyisha lililofurahiwa na rais wa umbile la Kiyahudi nchini Uturuki, hadi dhihirisho la urafiki aliopewa Bashar Assad nchini UAE, ambayo yalikuwa kama kumwaga chumvi kwenye kidonda cha Ummah mzima wa Kiislamu.

**Enyi Waislamu… Enyi Watu Wenye Nguvu na Ulinzi:**

Kafiri Magharibi isingeweza kufanya mashambulizi haya kama si watawala wa Kiislamu kufungua milango ya ardhi wazi kwa ajili ya kuwachezea wapendavyo. Kwa hiyo, upotovu huu wa maisha ya kibinafsi ya Umma wa Kiislamu hautasitishwa, isipokuwa uwe na Khalifa atakayewakusanya watu wake na kuwasaidia dhidi ya maadui zao, hivyo kuwasahaulisha minong'ono ya Shetani. Wamagharibi hawakutumia hatua hizi isipokuwa kwa sababu walitambua masuala mawili muhimu: La kwanza ni kwamba Umma wa Kiislamu bado unafanya uasi juu ya masharti yake na unataka kuregesha mamlaka yake na kuufukuza ushawishi wa Magharibi kutoka katika ardhi yake. Pili ni kwamba masuala ya Urusi na China yatawavuruga Wamagharibi kutoka katika nchi za Kiislamu, na kwa hiyo wakawakabidhi jukumu hilo watawala vibaraka. Hivyo basi, fursa imeiva kwa Ummah kujiondoa wenyewe kutoka kwa vibaraka wa Magharibi na khiana zao, kuachwa huru kutokana na ushawishi wao na kuichukua ardhi yake mikononi mwake. Jambo hili liko kwa watu wenye nguvu na ulinzi ndani yake, na msaada wa rai jumla miongoni mwao. Basi fanyeni hima, enyi Waislamu, katika mwezi huu uliobarikiwa, na muwasukume wenye nguvu na ulinzi miongoni mwenu kutoa Nusra (msaada wa kimada) kwa Uislamu, waweke mikono yao mikononi mwa Hizb ut Tahrir, kwa kutaraji kwamba Mwenyezi Mungu (swt) itatoa ushindi. Mwenyezi Mungu (swt) asema:

[يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا إِن تَنصُرُوا اللَّهَ يَنصُرْكُمْ وَيُثَبِّتْ أَقْدَامَكُمْ]

**“Enyi mlio amini! Mkimnusuru Mwenyezi Mungu naye atakunusuruni na ataithibitisha miguu yenu.”** [47: 7].

Ima hili, au mtazongwa na fedheha duniani na ghadhabu ya Mwenyezi Mungu (swt) kesho Akhera! Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) amesema:مَا مِنْ امْرِئٍ يَخْذُلُ امْرَأً مُسْلِماً فِي مَوْضِعٍ تُنْتَهَكُ فِيهِ حُرْمَتُهُ وَيُنْتَقَصُ فِيهِ مِنْ عِرْضِهِ إِلَّا خَذَلَهُ اللَّهُ فِي مَوْطِنٍ يُحِبُّ فِيهِ نُصْرَتَهُ، وَمَا مِنْ امْرِئٍ يَنْصُرُ مُسْلِماً فِي مَوْضِعٍ يُنْتَقَصُ فِيهِ مِنْ عِرْضِهِ وَيُنْتَهَكُ فِيهِ مِنْ حُرْمَتِهِ إِلَّا نَصَرَهُ اللَّهُ فِي مَوْطِنٍ يُحِبُّ نُصْرَتَهُ **"Hakuna mtu yeyote (Muislamu) atakayemtelekeza Muislamu mwengine katika sehemu ambayo heshima yake inachafuliwa na utu wake kukiukwa isipokuwa Mwenyezi Mungu atamtelekeza katika sehemu ambayo angependa kupata Nusra yake, na hakuna mtu yeyote (Muislamu) atakayemnusuru Muislamu mwengine katika sehemu ambayo heshima yake inachafuliwa na utu wake kukiukwa isipokuwa Mwenyezi Mungu atamnusuru katika sehemu ambayo angependa kupata Nusra yake."** [Imesimuliwa na Abu Dawood]. Hili ni kwa mtu mmoja, basi, enyi watu wenye nguvu na ulinzi, vipi kuhusu yule aliyefelisha Umma mzima wa bilioni mbili?! Mcheni Mwenyezi Mungu katika matukufu ya Waislamu, mcheni Mwenyezi Mungu kabla hamjachelewa.

Kwa kutamatisha, tunaulingania Umma wa Kiislamu katika mwezi huu mtukufu uufanye mwezi wa Ramadhan mwaka huu kuwa ni mwanzo mpya wa ahadi kwa Mwenyezi Mungu (swt), katika kufuata haki, hata kama Magharibi na vibaraka wake wanachukia, na wafurahie ushindi wa Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu (swt) asema:

وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُم فِي الأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَى لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْناً يَعْبُدُونَنِي لا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئاً وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَلِكَ فَأُولَئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ

**“Mwenyezi Mungu amewaahidi wale walio amini miongoni mwenu na wakatenda mema, ya kwamba atawafanya makhalifa katika ardhi kama alivyo wafanya makhalifa wa kabla yao, na kwa yakini atawasimamishia Dini yao aliyo wapendelea, na atawabadilishia amani baada ya khofu yao. Wawe wananiabudu Mimi, wala wasinishirikishe na chochote. Na watao kufuru baada ya hayo, basi hao ndio wapotovu.”** [An-Nur: 55].

Naomba mwezi wenu uwe wa baraka, Wassalamu Alaikum Wa Rahmatullah Wa Barakatuh.

**Mkesha wa Jumamosi siku ya kwanza ya mwezi mtukufu wa Ramadhan wa mwaka 1443 H.**

**Mhandisi Salah Eddine Adada**
**Mkurugenzi wa Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

# HABARI NA MAONI
# Kipimo cha Sarafu ya Dola ndio Chanzo cha Mfumuko wa Bei

**Habari:**

Imekuwa ni wiki ya majanga ndani ya Afrika Mashariki, kutokana na uhaba wa mafuta na kuzidi kwa bei za bidhaa za watumiaji, ilhali eneo likiendelea kujinasua kutoka katika janga la Covid-19 ili kuhuisha uchumi wa dola.

Maeneo mengi hivi karibuni yameshudia uhaba mkubwa wa mafuta, na pale ambapo bidhaa hiyo inapatikana, basi bei yake imepanda viwango vya juu mno.

Gharama ya maisha inazidi kupanda. Nchini Kenya mfumuko wa bei ni asilimia 6.29, Uganda ni asilimia 3.2, Rwanda ni asilimia 4.2, Tanzania ni asilimia 3.8, Burundi ni asilimia 13.3, Sudan Kusini ni asilimia 25 na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo ni asilimia 5. (*The EastAfrican, Saturday, 09/04/2022)*

**Maoni:**

Hali ya dhiki inayoendelezwa kutokana na kutiwa minyororo sarafu za mataifa mengine kwa ile inayodaiwa kuwa ni sarafu yenye nguvu ya Dola ya Amerika haingii akilini! Kwa hiyo, jambo hilo linathibitisha uhuru wa kiuhadaifu uliopo katika dunia hii inayotawaliwa na Amerika na taasisi zake za kifedha hususan Shirika la Fedha la Kimataifa na Benki ya Dunia.

Janga la Covid-19 na mzozo baina ya Urusi na Ukraine umezidisha kasi ya kuzama kwa nidhamu ya kiuchumi ya kirasilimali katika kina ambacho haitarajiwi kunusurika kwani kuanguka kwake kutakuwa na hatari zaidi ikilinganishwa na ile ya 2008. Utabiri mpya wa ukuaji wa uchumi umekitwa juu ya sarabi ili kuwalaza watu walioghadhabika lakini ni vipofu wa kimfumo.

Kuzidi kwa mfumuko wa bei SIO tu ndani ya nchi za Afrika Mashariki, bali duniani kote. Vyombo vya habari vya Magharibi ambavyo daima vinaegemea upande mmoja vimelazimika kupeperusha kuzidi kwa gharama ya maisha inayowakumba raia katika yale yanayoitwa mataifa ya ulimwengu wa kwanza na pili. Yote ikiwa ni natija ya utumwa wa sarafu zao kwa dola. Ama kuhusiana na mataifa ya ulimwengu wa tatu hususan Afrika, yanataabika zaidi kutokamana na utumwa wao wa kikoloni hadi leo!

Kwa mfano nchini Kenya, hivi sasa Dola inabadilishwa dhidi ya shilingi ya Kenya kwa $1 = Ksh117! Tunapouweka muktadha huo katika mahusiano ya Kenya katika usafirishaji bidhaa kutoka ng'ambo na madeni yake ya nje ni janga kubwa. Katika nchi nyingine, hali ni mbaya zaidi. Yote haya ni natija ya kipimo cha sarafu ya dola ambayo haidhaminiwi kwa chochote kile isipokuwa kuwa na matumaini katika Amerika iliyoimarika! 'Matumaini' ni kipimo katika nidhamu ya fedha za makaratasi!

Kama Waislamu lazima tusikate tamaa kwa sababu tunayo nidhamu ya kiuchumi ya Kiislamu ambayo imechipuza kutoka kwa Mummba wa ulimwengu, uhai na mwanadamu –Allah(swt). Badala yake tunatakiwa kuelekeza nishati yetu na kuhimili kipindi hichi cha ugumu wa kiuchumi uliozidishwa na kufeli kwa mamlaka ya Amerika na mfumo wake batili wa kirasilimali wa kisekula na nidhamu zake zinazojumuisha sio tu nidhamu kandamizi ya kiuchumi iliyojikita juu ya utozaji ushuru na mikopo ya riba.

Sasa ni wakati wa Waislamu kuwasilisha Uislamu kuwa ni mfumo mbadala ambao una uwezo wa kutatua matatizo yaliyopenya katika nyanja za maisha. Hilo litawezekana kupitia uongozi wenye uwezo wa Dola ya Kiislamu, Khilafah iliyosimamishwa tena kwa njia ya Utume. Khilafah itautekeleza Uislamu kiukamilifu na hususan nidhamu yake ya kiuchumi ambapo ***sarafu ya dhahabu na fedha*** itatumika kama kipimo cha kifedha na sio chengine kile! Kwa kuongezea, itafutilia mbali utozaji ushuru watu kwa kuwa Uislamu unalizingatia hilo kuwa ni ukandamizaji kwa njia ya kuwapora mali zao walizo zichuma kwa dhiki. Ama kuhusu riba na aina zake zote haitoruhusiwa. ﴿وَأَحَلَّ ٱللَّهُ ٱلْبَيْعَ وَحَرَّمَ ٱلرِّبَوٰاْ﴾ **"Lakini Mwenyezi Mungu ameihalalisha biashara na ameiharamisha riba." [Al-Baqarah 2: 275].** Kwa kuongezea, itajifunga na sera za kujitosheleza kindani ili kuepuka utegemezi wa ng'ambo.

Kujiunga na ulinganizi wa kurudisha tena maisha ya Kiislamu kupitia kusimamisha tena mradi wa Khilafah ndio suluhisho pekee kwa matatizo tofauti yanayo wakabili wanadamu duniani kote. Kuwabadilisha wanasiasa wa kidemokrasia, vyama vyao au kubadilisha katiba au kujiunga na Muungano wa Afrika (AU) au Umoja wa Mataifa (UN) au mifano yake hakutoleta afueni katika hali zetu, kwa sababu chanzo ni wao kuwa watumwa kwa mfumo wa kirasilimali wa kisekula na nidhamu zake zenye sumu. Majanga yataendelea pasina kusita isipokuwa tubadilishe demokrasia, nidhamu ya utawala wa kubahatisha na sehemu yake ichukuliwe na ile ya Khilafah.

**Imeandikwa kwa ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Ali Nassoro Ali**
**Mwanachama wa Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

# HABARI NA MAONI
# Katika Vita vya Urusi na Ukraine: Afrika Haipaswi Kumuunga Mkono Yeyote



**Habari:**

Vita vinavyoendelea kati ya Urusi na Ukraine vinaonekana kuigawa Afrika juu ya kuunga mkono upande gani na kwa nini? Viongozi wengi wa Afrika wameamua kutofungamana na upande wowote huku wachache baadhi yao wakionesha wazi pande zao. Licha ya misimamo binafsi ya nchi, Umoja wa Afrika (AU) ulituhumu uvamizi wa Moscow na kutoa mwito wa kusitisha mapigano mara moja. Raisi wa Senegal Macky Sall ambaye ni Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika na Mwenyekiti wa Tume ya Umoja wa Afrika Moussa Faki Mahmat wanaitaka Urusi kuheshimu sheria za kimataifa na mamlaka huru ya nchi ya Ukraine.

**Maoni:**

Kama tukitazama pande mbili za mgogoro huu, yaani Urusi na Ukraine ambayo inaungwa mkono na Ulaya na Amerika, ni wazi kuwa hakuna anayepaswa kuungwa mkono. Vita halisi hapa ni kati ya Urusi upande mmoja, na Ulaya na Amerika hususan katika upande mwingine, huku Ulaya na Amerika ikiitumia Ukraine kama mbuzi wa kafara.

Kwa hivyo, ikiwa mjadala wetu utakuwa katika wahusika wakuu wa vita hii, yaani Urusi, Ulaya na Amerika, nukta zifuatazo za mjadala ni lazima zihusishwe ili tuweze kujua ni upande upi wa mgogoro au ni msimamo upi Afrika inatakiwa ichukue kuhusu vita hivi vinavyoendelea.

Nchi za Ulaya ambao wanaunga mkono Ukraine ili kudhibiti ushawishi wa Urusi hawana maana. Ni wanafiki, wenye historia ndefu ya uvamizi, ukatili, na umwagaji wa damu za Waafrika.

Walisababisha kupotea kwa watu milioni 100 na vifo milioni 12.5 katika Afrika katika kipindi cha utumwa kabla ya ukoloni wa kinguvu. Katika karne za biashara ya utumwa ya Kuvuka Atlantiki inakadiriwa takribani watu milioni 100 walitolewa katika makaazi yao (Dr Sheila S. Walker: Faces and Voices of the African Diaspora, USA, 2008). Katika kipindi hicho inakadiriwa Afrika ilikuwa na watu takribani milioni 62.2 mwaka 1500 na mwaka 1900 walikuwa karibu milioni 140.755,000 pekee.

Baada ya utumwa, nchi za Ulaya zilikoloni kwa mabavu Afrika na kuweka sera kandamizi za kimabavu za kufanyisha kazi na kodi, sheria kandamizi za udhibiti wa kumiliki ardhi na baadaye unyonyaji wa rasilimali uliochangia Afrika kudumaa kimaendeleo kwa Afrika huku wakilifanya Bara Ulaya kusonga mbele kwa

*Endelea... UK 7*


Email: info@uqab.or.ke

kiwango kikubwa.

Ulipokuja uhuru wa bendera, Ulaya na Amerika waliendelea kupambana kuigawa tena Afrika na kuendelea kulinda ushawishi wao kupitia ukoloni mamboleo.

Afrika ilikumbwa na mapinduzi na vita vingi vya wao kwa wao vilivyosababishwa na ushindani kati ya Ulaya na Amerika, kila mmoja wao akitaka kuweka kibaraka wake katika utawala.

Kupitia ukoloni mamboleo, Amerika na Ulaya waliitengeneza Afrika utegemezi kupitia Mfuko wa Fedha wa Kimataifa na Benki ya Dunia na kupitia biashara kwa mfumo usio wa haki kwa mbinu ya soko huria. Amerika na Ulaya wanatumia misaada na mikataba ya kilaghai ya kibiashara kama 'ramba ramba tamu' baina ya Afrika na nchi zao.

Kuhusu Urusi, ni kweli kuwa haikuwahi kulikoloni Bara la Afrika moja kwa moja, lakini katika kipindi cha zama za Usovieti ilisambaza kwa kulazimisha mfumo wake wa Ujamaa uliosababisha majanga mengi na umwagaji damu katika kusambazwa katika mchakato huo.

Kulikuwa na vita vingi vilivyopiganwa kwa niaba yao katika kipindi cha Vita Baridi kati ya Usovieti na Amerika, mfano Vita vya Ogaden nchini Somalia (1977-1978) na Vita vya Wenyewe kwa Wenyewe nchini Angola (1975-2002) vikiwa na malengo ya kupanua wigo wa ushawishi wa Usovieti, ambavyo viliiathiri Afrika kwa kupelekea, vurugu mauaji na kukosekana utangamano.

Kwa sasa Urusi inahuisha tena maslahi yake ndani ya Afrika si kwa ajili ya kueneza mfumo wake baada ya kushindwa mfumo wake wa Ujamaa dhidi ya ubepari, bali ni kwa ajili ya unyonyaji wa kiuchumi, kwani Urusi tayari imeshachukua mfumo wa ubepari.

Biashara ya silaha ya Urusi kwa Afrika na vifaa vya kijeshi inachukua zaidi ya asilimia 50 ya biashara yake na Afrika. Katika mkutano wa Sochi mwaka 2019, vifaa vya kijeshi vilitawala maonesho hayo.

Makampuni yenye uhusiano na Kremlin kama Gazprom, Alrosa, Rosatom na Rosneft yanahusika kuendesha migodi ya madini na nishati nchini Angola, Algeria, Ghana, DRC, Msumbiji, Namibia, Afrika Kusini, Zimbabwe, nk. Biashara kati ya Urusi na Afrika ilifikia dolari bilioni 17.4 mwaka 2017.

Hivyo, washirika wa Ukraine yaani Ulaya na Amerika kwa upande mmoja, na Urusi upande mwingine, makundi yote mawili yana ajenda ya unyonyaji kwa Afrika.

Kulaani kwa nchi za Magharibi dhidi ya uvamizi wa Urusi nchini Ukraine ni wa kinafiki, na Afrika haipaswi kuunga mkono upande wowote. Unafiki mwingine wa wazi wa Wamagharibi ni kuhusu ubaguzi wa wakimbizi. Licha ya ukweli kuwa Urusi, Ulaya na Amerika ndio wanaotengeneza vita vingi katika Afrika, na kufaidika na vita hivyo na migogoro hiyo isiyokwisha, bali pia wamekuwa wakiwabagua kwa ukatili wahanga na wakimbizi kutoka Afrika kama ilivyo kwa wakimbizi kutoka Mashariki ya Kati. Imeripotiwa kuwa ndani ya robo ya kwanza ya mwaka 2021, zaidi ya nusu ya watu walioingia Italia kutokea Tunisia ambao wengi ni raia kutoka nchi za Afrika za Kusini mwa Jangwa la Sahara na kiasi cha wahamiaji 453 walikufa wakijaribu kuingia Ulaya kutokea Afrika Kaskazini kutokana na kuzuiwa, kubaguliwa na mazingira magumu wanayopata katika kuingia Ulaya.

Ummah wa Kiislamu katika Afrika unapaswa kutambua kuwa wote Ulaya, Amerika, Urusi na Ukraine wanahusika na umwagaji damu wa kaka zetu na dada zetu wa Kiislamu. Mifano ya karibuni zaidi ni uvamizi wa Amerika kwa Iraq wa mwaka 2003 uliopelekea vifo zaidi ya Waislamu milioni 1.2 vita ambavyo Amerika, Ulaya, ikiwemo na Ukraine zilishiriki kwa kutuma zaidi ya wanajeshi 5,000 nchini Iraq.

Pia walivamia Afghanistan mwaka 2001 na kuua watu zaidi ya nusu milioni, Ukraine iliruhusu Amerika na Washirika wake kutumia anga na kambi zake za kijeshi pamoja na kutoa wanajeshi. Urusi pia haina tofauti na wenzake katika hili, imeua mamilioni ya Waislamu katika kipindi cha mfumo uliofeli wa Ujamaa. Nchi zote za Kiislamu zilizokuwa sehemu ya Umoja wa kiSovieti zilishuhudia mauaji ya kutisha, mateso, kufungwa kwa misikiti nk. Urusi imeuwa wengi Afghanistan na inaendelea na mauaji ya halaiki katika Syria, Libya nk. Bila ya kusahau namna inavyofunga Waislamu wanaolingania Uislamu.

Kwa hivyo, kwa Waislamu popote walipo, kwa kuunga mkono Urusi ni kama kuunga mkono Ukraine, Ulaya na Amerika kwa sababu makundi yote mawili ni wauwaji wa kaka zetu na dada zetu.

Hali ya ushindani wa kimataifa kati ya Mabepari kama Amerika, Ulaya, Urusi na China juu ya mrundo wa rasilimali ya mafuta na madini ya Afrika inalazimisha hitajio la haraka la kurejeshwa kwa dola ya uadilifu ya Khilafah, ili kuliokoa bara hili na kuliinua juu ili kuwa na sauti na maamuzi huru katika kadhia za kimataifa.

**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Said Bitomwa**
**Mwanachama wa Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir Tanzania**

Afisi kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir

بسم الله الرحمن الرحيم

﴿وعد الله الذين آمنوا منكم وعملوا الصالحات ليستخلفنهم في الأرض كما استخلف
الذين من قبلهم وليمكنن لهم دينهم الذي ارتضى لهم وليبدلنهم من بعد خوفهم أمنا
يعبدونني لا يشركون بي شيئا ومن كفر بعد ذلك فأولئك هم الفاسقون﴾

KUMB: 29/1443 | Jumapili, 2 Ramadhan 1443 H | 03/04/2022 M


**Taarifa kwa Vyombo Vya Habari**

# Bangladesh Yazifunga Shule za Waislamu wa Rohingya Yatishia Kuwavua Kitambulisho Chao na Kuwahamisha hadi Kisiwa cha Mbali Endapo Zitafunguliwa

Maafisa nchini Bangladesh wanatishia kuwanyang'anya wakimbizi wa Rohingya hati zao za utambulisho na kuwahamisha kwa nguvu hadi katika kisiwa cha mbali ambacho hukumbwa na mafuriko ya mara kwa mara, endapo watakiuka marufuku jumla kwa shule walizozianzisha, kulingana na shirika la Human Rights Watch. Ripoti iliyotolewa na shirika hilo ilisema kuwa wakimbizi wanahitaji hati za utambulisho zinazoitwa "kadi za data" zilizotolewa na shirika la Umoja wa Mataifa la kuhudumia wakimbizi kwa ushirikiano na serikali ya Bangladesh ili kupata misaada na huduma za kimsingi. Tangu Disemba 2021, mamlaka za Bangladeshi zimepiga marufuku shule zilizoanzishwa na walimu wa Rohingya ili kufidia ukosefu wa elimu rasmi na ya sekondari katika kambi za wakimbizi, kufungwa kwa shule za Kiislamu, na kupigwa marufuku mashirika ya kibinadamu kutoa elimu kwa watoto wakimbizi wa Rohingya nje ya madarasa ya msingi na yasiyo rasmi na ngazi ya msingi.

Utaratibu mpya wa uhalifu unafanywa na mamlaka za Bangladesh dhidi ya ndugu na dada zetu wa Rohingya ambao wametafuta hifadhi huko ili kuepuka ukatili na uhalifu wa Wabudha dhidi yao. Inawazuia na kuwashinikiza katika riziki zao ikiwa ni pamoja na riziki za familia zao kwa kutishia kuwapokonya vitambulisho vyao vinavyotumika kupokea msaada. Juu ya hayo wanatishia kuwahamishia katika kisiwa kingine cha mbali ambacho hukumbwa mafuriko na vimbunga vya mara kwa mara, ambacho ilihamisha watu 20,000 hapo awali, si kwa jengine isipokuwa kwamba wakimbizi hao wa Rohingya walitaka kuwafundisha watoto wao juu ya Dini yao na sayansi za kiulimwengu, hivyo wakaanzisha shule za kujaza upungufu wa idadi ya shule, ambapo mamlaka ilizifunga, na kuwatishia walimu na walezi kutofundisha kwa siri majumbani mwao.

Shirika la kutetea haki za binadamu la Human Rights Watch limetahadharisha kuwa takriban watoto 30,000 watanyimwa elimu kutokana na hatua hizo, jambo linalomaanisha kupotea kwa kizazi kizima, kana kwamba watoto hao hawajaonja ukandamizaji na dhuluma za kutosha wanazokabiliana nazo nchini mwao, pamoja na uchungu wa hifadhi na ugumu wa njia yake, na ugumu wa kuishi katika kambi, kiasi kwamba wananyimwa elimu baada ya kupata njia ya kuifikia.

Mamlaka za Bangladesh zinadai kwamba zimechukua hatua hizi kwa lengo la kuziondoa shule "zinazopigia debe itikadi kali na kushiriki katika vitendo haramu." Kwa hiyo, walimwaga hasira zao kwa shule za Kiislamu na kuzifunga. Ni kisingizio dhaifu na kipimo kilichowekwa wazi katika vita na uadui wake kwa Uislamu na Waislamu na ukaribu wao kwa makafiri katika vita vyao viovu dhidi ya Uislamu na Waislamu chini ya kauli mbiu ya "Kupambana na Ugaidi na Itikadi kali."

Imedhihirika kwa kila mwenye macho na utambuzi kuwa utawala wa Kibengali na tawala nyinginezo katika nchi za Waislamu zimesaliti na kula njama dhidi ya masuala yao. Ni wakati muafaka sasa wa kuzipindua tawala hizi vikaragosi na kuzibadilisha kwa mfumo wa Kiwahyi, unaotabikisha Dini na kuwapa haki waliodhulumiwa na kukomesha mateso yao. Ni Khilafah Rashida ya pili pekee ndio inayoweza kufikia hili. Basi jitokezeni muisimamishe.

Enyi watu wenye nguvu na ulinzi: Mnusuruni Mwenyezi Mungu, Mtume Wake, na waumini, na Mwenyezi Mungu atawanusuru hapa duniani na kesho Akhera.


**Kitengo cha Wanawake**
**katika Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**




Email: info@uqab.or.ke

JIBU LA SWALI

# Matarajio ya Wakoloni Nchini Tanzania




**Swali:**

Tanzania ni miongoni mwa nchi zenye utulivu zaidi wa kisiasa barani Afrika. Tanzania inacheza dori katika Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC). Uhusiano wake na mkoloni wake wa zamani Uingereza ni imara. Lakini tunaona harakati za Marekani na China ndani yake. Je, ni kipi kiwango cha ushawishi wa Marekani na China katika nchi hii? Je, kuna mzozo wa kimataifa ndani yake? Na kwa nini kundi la SADC lilianzishwa?

**Jibu:**

Ili kupata jibu wazi kwa maswali hayo hapo juu, tunahakiki mambo yafuatayo:

**Kwanza:** Tanzania ni nchi ya Kiislamu, asilimia ya Waislamu ndani yake inazidi 60%. Uislamu uliingia humo mwishoni mwa karne ya kwanza ya Hijri, lakini ulikabiliwa na mashambulizi ya wakoloni, maadui wa Uislamu, kuanzia ukoloni wa Wareno hadi ukoloni wa Wajerumani na Waingereza, na Marekani sasa iko kwenye njia ya kuingilia kati... Eneo lake la kimkakati linaifanya kuwa muhimu kwa nchi za kikoloni, iko kwenye Bahari Hindi kutoka kwenye mipaka yake ya mashariki, na iko ndani ya eneo la Maziwa Makuu ya Afrika. Kwa sababu hiyo, ulikuwa ni mlango mmojawapo wa wakoloni kupenya kwenye kina kirefu cha Afrika na kuikoloni. Tanzania ilipata uhuru wake rasmi mwishoni mwa 1961, lakini ushawishi wa Waingereza uliendelea kuitawala.

**Pili:** Uingereza ilimteua Julius Nyerere kama rais wa Tanganyika, ambaye alionekana kuongoza harakati za ukombozi dhidi ya ukoloni! Hapo awali aliteuliwa kuwa waziri katika serikali ya Uingereza iliyoendesha eneo hilo kabla ya uhuru. Zanzibar ilitwaliwa na Tanganyika mwaka 1964, ili kuunda Muungano wa Tanzania, kwa mujibu wa mpango wake, iliouandaa kusimama dhidi ya Marekani, ambayo ilianza kufanya kazi ya kuchukua nafasi ya ukoloni mkongwe barani Afrika. Nyerere alitawala Tanzania kwa chuma na moto hadi 1985, akiunganisha ushawishi wa Waingereza na kupiga vita Uislamu. Alikuwa akijificha nyuma ya kauli mbiu ya mapinduzi na ujamaa katika wakati ambapo alikuwa akitabikisha mfumo wa kirasilimali kama ilivyo desturi ya mawakala wengi wa nchi za Magharibi.

**Tatu:** Kwa sababu Waislamu ndio wengi (zaidi ya 60%), na ili rais asitokee kwao, iwapo kungekuwa na uchaguzi wa rais, waliweka katiba inayotamka katika ibara ya tatu ya Kifungu cha 47 kwamba "Ni

*Endelea... UK 10*


Email: info@uqab.or.ke

lazima mgombea urais awe anatoka sehemu fulani ya muungano (Tanganyika au Zanzibar). Wakati huo huo, naibu anapaswa kutoka upande mwingine ". Kuna ufahamu na sio utaratibu wa kikatiba kwamba marais wakristo na waislamu wapishane. Baada ya kifo cha Rais Mkristo Julius Nyerere, aliyetawala kwa muda mrefu zaidi, kuanzia mwisho wa 1961 hadi 1985, Hassan Mwinyi mwenye asili ya Kiislamu alichukua madaraka (1985-1995), kisha Mkristo Benjamin William (1995-2005). na ndipo Rais Mrisho Kikwete mwenye asili ya Kiislamu akashika madaraka (2005-2015), kisha Mkristo akaingia madarakani, John Magufuli na akafariki mwaka jana. Baada ya hapo, naibu wake, Samia Hassan, mwenye asili ya Kiislamu, alichukua kiti cha urais tarehe 19/3/2021.

Samia Hassan alikuwa waziri katika serikali ya Zanzibar ndani ya Muungano. Mnamo 2014, aliteuliwa kuwa Waziri wa Nchi kwa Masuala ya Muungano. Mwaka 2015, Rais John Magufuli alimchagua kuwa Makamu wa Rais, akiwapiku wengi kutoka Chama Cha Mapinduzi (CCM), Chama tawala cha Nyerere, kilichokuwa madarakani pekee, mara zote kilishinda kwa asilimia kubwa. Katika uchaguzi uliopita wa urais uliofanyika mwaka 2020, chama cha Nyerere kilishinda kwa 84.39%, na kisha mgombea wake Magufuli na makamu wake, Samia Hassan akashinda awamu ya pili, na hii inaashiria kuwa watawala wa Tanzania bado wanaifuata Uingereza, kwa sababu chama hicho tiifu kwake, chama cha Nyerere, bado kinatawala serikalini. ... Ili kuendeleza utamaduni uliokubalika wa kisiasa wa kupokezana madaraka, Samia Hassan alimteuwa aliyekuwa rais msaidizi wa zamani wa masuala ya uchumi, Philip Mbango, kuwa naibu wake ambaye ni Mkristo. Kumbuka kwamba rais Samia Hassan alizaliwa Januari 1960 nchini Zanzibar, ambayo inafurahia uhuru nusu wa utawala, na idadi ya Waislamu ndani yake ni karibu 99%. Baadaye niliendelea na masomo ya Utawala wa Umma kwanza nchini Tanzania kisha nikahitimu Chuo Kikuu cha Manchester, Uingereza. Alikula kiapo cha kikatiba akiwa amevaa hijabu na Qur'an mkononi mwake wa kulia, hivyo akajipatia sifa njema miongoni mwa watu wa nchi yake ya Waislamu, hasa kwa vile alifuata njia isiyo ya kugombana na upinzani.

**Nne:** Uingereza inaitazama Tanzania kwa kiasi fulani cha umuhimu kutokana na nyanja ya kisiasa na kiuchumi.

Ama kipengele cha kisiasa, eneo lake kama moja ya milango ya kuingia kwenye kina kirefu cha Afrika na ukoloni wake kunaifanya kuwa muhimu kwao. Uingereza imefanya kazi ya kusimama dhidi ya kuenea kwa Uislamu na kuupiga vita na watu wake wanaomkataa mkoloni na kukabiliana naye. Uingereza kuipoteza Tanzania kulisababisha ipoteze baadhi ya nchi jirani, ambazo Uingereza bado ina ushawishi ndani yake kama Kenya, Malawi, Zambia na nchi nyingine katika eneo hilo.

Kwa upande wa kiuchumi, ni mwekezaji mkubwa wa kigeni wa moja kwa moja nchini Tanzania katika sekta za madini, viwanda na uzalishaji wa kilimo, na mwekezaji mkubwa wa chai ya Tanzania, na mauzo yake ya nje ndiyo yanatawala soko la Tanzania, hasa magari na vifaa vya kielektroniki.

**Tano:** Kadhalika, Marekani inaitazama Tanzania kwa kiwango fulani cha umuhimu na inajaribu kupata mwanya wa kuifikia kwa njia zote, na kubadilisha ukoloni mkongwe. Tanzania ilikuwa miongoni mwa nchi chache za kiafrika ambazo marais wa Marekani walizizuru kwa ajili ya kuonesha nia yake na kujaribu kuivutia Marekani... Hivyo Bush Mwana alizuru Tanzania mnamo tarehe 17/2/2008. Vilevile Obama mnamo tarehe 1/7/2013, alipoweka jiwe la msingi la kumbukumbu mbele ya ubalozi wa nchi yake kwa heshima ya Wamarekani kumi na moja waliouawa katika shambulizi la bomu la mwaka 1998 katika ubalozi wa Marekani jijini Dar es Salaam.

**Sita:** Kwa hivyo, inaweza kusemwa kwamba mzozo wa kisiasa unaendelea kati ya Uingereza, mkoloni mkongwe anaye endelea, na Amerika, ambayo inajaribu kupenya ndani ya Tanzania ili kufanikiwa ushawishi wa Kiingereza, na nchi zote mbili zinatumia njia zao mbaya za kikoloni kufikia malengo yao.

1- Kwa upande wa Amerika, imetangaza kupinga matokeo ya uchaguzi wa 2020. Morgan Ortagus, msemaji wa Wizara ya Mambo ya Nje ya Marekani, aliandika mnamo tarehe 30/10/2020 baada ya kutangazwa kwa ushindi wa Rais Magufuli. Aliandika kwenye akaunti yake ya Twitter, akisema kwamba "alikuwa na wasiwasi kuhusu ripoti za kuaminika za dosari katika uchaguzi na matumizi ya nguvu dhidi ya raia wasio na ulinzi." Alisema, "Tutawajibisha watu binafsi kwa hili." Pia, Amerika inatabanni matakwa ya upinzani, haswa Chama cha Chadema. Huku ni kuleta machafuko ya kisiasa ili kuweza kuvunja utawala wa chama tawala, Chama cha Uingereza... Kumbuka kuwa upinzani bado ni dhaifu. Mgombea wa chama kikubwa cha upinzani cha Democratic and Progress Party (Chadema) hakupata asilimia kubwa katika uchaguzi wa urais uliofanyika mwaka 2020. Mgombea wake Tundu Lissu alipata 13.03%. Mgombea wa Chama cha Chadema aliyakataa matokeo hayo na kusema "kilishuhudia udanganyifu usio na kifani katika historia yetu..." Kadhalika, Marekani inapatiliza wito wa kujitenga, hasa wito wa kujitenga kwa Zanzibar na Tanganyika... Inatumia Mfuko wa Fedha wa Kimataifa kama njia ya kuishawishi serikali nchini Tanzania!

2- Kwa upande wa Uingereza, inafanya kazi kwa mujibu wa mbinu yake chafu ya kisiasa kufunga milango ambayo Marekani inajaribu kuipatiliza nchini Tanzania, kwa upande mmoja inaonekana kukubaliana na Marekani, na kwa upande mwingine inafuata sera tofauti.

a- Kuhusu uchaguzi, Uingereza ilitoa tamko kuhusu hilo. Waziri wa Uingereza wa Masuala ya Afrika,

***Endelea... UK 11***

James Doddridge, alisema kwenye akaunti yake ya Twitter mnamo tarehe 30/10/2020, ("Uingereza ina wasiwasi kuhusu habari kuhusu dosari" na kutoa wito wa "uchunguzi wa wazi" na kuhimiza vyama vya kisiasa "kutafuta suluhisho la amani"), Amerika iliridhika, lakini haikupinga matokeo ya uchaguzi, wala haikusema yale ambayo Amerika ilisema: (kwamba kuna ripoti za kuaminika za ukiukaji wa uchaguzi) au wito wa (uwajibikaji kwa wale waliohusika)!

b- Kwa upande wa upinzani, viongozi wa kundi la Kiislamu lililotaka uhuru kamili wa eneo lenye uhuru nusu wa kujitawala la Zanzibar nchini Tanzania walifutiwa mashtaka ya ugaidi: [Viongozi mashuhuri wa jumuiya ya kiraia, Jumuiya ya Uhamasishaji na Ulinganizi wa Kiislamu, au UAMSHO, waliachiwa huru baada ya kukaa kizuizini kwa miaka minane, Farid Hadi na Mselem Ali Mselem waliachiliwa Jumanne usiku, na Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma, Sylvester Mwakitalu, aliwathibitishia waandishi wa habari kwamba mashtaka yote dhidi yao yamefutwa..." (https://apnews.com/)] na pia katika wiki za hivi karibuni iliruhusiwa kwa baadhi ya magazeti ya Kiswahili yaliyopigwa marufuku kuregelea uchapishaji, na Rais Samia Suluhu Hassan amewasamehe wafungwa wengi wa dhamiri, wakiwemo wanachama wa Chadema.

c- Kuhusu suala la Mfuko wa Fedha wa Kimataifa, licha ya ukweli kwamba IMF ilifukuzwa Tanzania enzi za Rais Hassan Mwinyi, kwa sababu ilitaka kumwekea masharti kama vile kushusha thamani ya sarafu, kupandisha bei na kufungia mishahara, ambayo huongeza mateso ya watu, kama IMF inavyofanya katika kila nchi inayoomba mkopo. Hata hivyo, IMF ilichukua fursa ya athari za janga la virusi vya Korona kutoa mkopo kwa Tanzania wenye thamani ya dolari milioni 567, ikisema kuwa "mkurupuko wa virusi vya Korona ulisababisha kuporomoka kwa sekta ya utalii na kuzidisha haja ya ufadhili mkubwa." (Bloomberg 8/9/2021), hivyo serikali ya Tanzania ilikubali kuchukua mkopo huo, huku ikijua kuwa Tanzania haiutambui mkurupuko huo wa Korona na haikuweka hatua za kuzuia, lakini ilikubali kuboresha uhusiano na IMF na sio kugongana na Amerika, sambamba na mtazamo wa Uingereza inayoifuata!

d- La muhimu zaidi ni kuanzishwa kwa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC), ambayo ilianzishwa mnamo tarehe 17/8/1992 badala ya Kongamano la Uratibu wa Maendeleo ya Kusini mwa Afrika, iliyoanzishwa nchini Botswana mnamo tarehe 1/4/1980 kutoka nchi wanachama tisa (Angola, Botswana, Lesotho, Malawi, Msumbiji na Eswatini, Tanzania, Zambia na Zimbabwe) na sasa ni 15 baada ya kujiunga Afrika Kusini, Namibia, Mauritius, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Madagascar, na Ushelisheli na ilianzishwa na Uingereza ili kudumisha ushawishi wake katika eneo hilo, na kuzuia kuingilia katika kwa ushawishi wa Marekani katika nchi za kikundi hilo. Hivyo basi, pindi kampuni ya mafuta ya Marekani, Anadarko, ilipogundua hifadhi kubwa ya gesi asilia iliyoko katika Bonde la Rovuma, lililoko karibu na pwani ya mkoa wa Cabo Delgado kaskazini mwa Msumbiji mwaka 2010, ambako Waislamu wanaishi nchini humo.

Kisha hifadhi hii ilithibitishwa mnamo mwaka wa 2017, kwa mujibu wa makala yaliyochapishwa na Financial Times mwaka 2017. "Gesi iligunduliwa katika vitaru viwili vya karibu, na kila moja yao kimethibitisha hifadhi ya futi za ujazo trilioni 75, ambayo ni ya kutosha - kulingana na wataalamu - kuisambazia Uingereza, Ufaransa, Ujerumani na Italia kwa zaidi ya miaka 20." Kwa hivyo, gesi ilipogunduliwa na kuthibitishwa mnamo 2017, Uingereza iligundua tabia ya Amerika ya kuingilia Msumbiji, haswa kwamba hii iliambatana na vuguvugu la uasi katika nchi hii lililozidi kuongozwa na kikundi cha ndani kiitwacho Ansar al-Sunna wal Jama'a, na kisha Rwanda, ambayo ina uhusiano na Amerika, ilijitolea kuisaidia Msumbiji dhidi ya (uasi) na kuijaribu kwa hili, Msumbiji ilikubali... Manmo tarehe 9/7/2021, Rwanda ilipeleka kikosi cha wanajeshi 1,000 kwa ombi la Msumbiji kusaidia kuzima waasi wa muda mrefu wa Kiislamu katika mkoa wa kaskazini wa Cabo Delgado... Ingawa Rwanda inashirikiana na Amerika, Msumbiji ilipendelea kuomba msaada kutoka Rwanda!

**Saba:** Uingereza ilipoona hili, ililisukuma kundi la SADC kurekebisha hali ya Msumbiji, ambayo ni mwanachama wake:

1- Viongozi wa SADC wakati wa mkutano walizipongeza nchi wanachama kwa kujitolea kwao kupeleka Kikosi cha Kudumu cha SADC na kutoa msaada wa kifedha katika Mkoa wa Cabo Delgado, kaskazini mwa Msumbiji, kwa ajili ya kutumwa nchini humo. (https://africa.sis.gov.eg 21/8/2021)

2- Pindi Rwanda mfuasi wa Marekani ilipopeleka wanajeshi 1,000 kaskazini mwa Msumbiji, ambayo si mwanachama wa SADC, idadi kadhaa ya wanachama wa SADC walipinga: ["Kutumwa kwa vikosi vya Rwanda kuliwakasirisha baadhi ya wanachama wa SADC, kwa kuwa ushiriki wa Rwanda hauko chini ya udhibiti wa SADC..." Walisema kwamba hoja ya uhalalisha ya Rwanda ambayo si mwanachama wa SADC, kwa msaada wa Msumbiji, ni kuhalalisha "kichocheo cha maafa" (https://www.defense-network.com 22/7/ 2021)].

Hivyo Uingereza, kwa kutambua majaribio ya Amerika kuingilia kati kupitia msaada wa Rwanda kwa Msumbiji, ilipotambua hilo mara moja ilituma msaada wa kijeshi kwa Msumbiji kupitia shirika lake la SADC ili Rwanda isibaki peke yake huko.

3- Kulingana na ripoti ya tovuti ya Bloomberg, [Waziri wa Mambo ya Nje wa Afrika Kusini alisema katika mkutano wa Kundi la nchi saba zilizoendelea kiviwanda: “Nilipata fursa ya kukutana na Ufaransa, Muungano wa Ulaya na Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani na kuwaeleza kuwa maoni yetu ni kwamba Jumuiya ya

***Endelea... UK 12***

Maendeleo ya Kusini mwa Afrika inapaswa kuongoza katika suala hili" (https://www.bloomberg.com/news/newsletters/13/8/2021)].

4- Hivi majuzi, kundi hilo lilifanya mkutano mnamo tarehe 18/1/2022 nchini Malawi kusaidia ujenzi wa kiuchumi na kijamii wa Cabo Delgado, ambayo ina utajiri mkubwa wa gesi asilia nchini Msumbiji, yenye wakaazi wapatao milioni 30, na idadi ya Waislamu karibu 20%. Kiasi cha gesi ndani ya mkoa huu inakadiriwa kuwa mita za ujazo trilioni 75. Mkutano huo uliidhinisha uungwaji mkono wa Msumbiji na hatua za kuimarisha amani, usalama na ufufuaji wa kijamii na kiuchumi katika mkoa huu ambako vuguvugu la kisilaha linafanya kazi. Kundi hilo liliapa kuendelea kupambana na ugaidi na watu wenye itikadi kali nchini Msumbiji. Rais Lazarus wa Malawi, ambaye ni mwenyekiti wa jumuiya ya SADC, alisema: ["Kujitolea kwa kundi hili ni kuhakikisha kuwa eneo la Cabo Delgado nchini Msumbiji linaendelea kuwa sawa, shwari na salama, na kwamba mkutano huu unatoa fursa ya kupitia kuhakiki misheni ya SADC nchini Msumbiji katika mapambano dhidi ya ugaidi." (SPA 18/1/2022)].

**Nane:** Kuhusu juhudi za China, hadi sasa imetawaliwa na ushawishi wa kiuchumi zaidi kuliko kufikia ushawishi wa kisiasa, na kuridhiana nayo kiuchumi ni kuiudhi Marekani. Kwa kuzingatia jambo hili inabainika kuwa Tanzania inajitahidi kuimarisha mahusiano yake ya kiuchumi na China ili kuokoa hali ya kiuchumi na hata kuepukana na utawala wa Mfuko wa Fedha wa Kimataifa juu yake, yaani utawala wa Marekani juu yake, yote ni kwa maelekezo ya Uingereza. Kwa sababu hii, Tanzania ilitia saini mikataba ya ushirikiano wa kiuchumi na kiufundi na China ili kufadhili miradi ya China nchini Tanzania. Kuna mazungumzo ya kufadhili miradi yenye thamani ya mabilioni ya dolari, ima ni kujenga bandari mpya kwa thamani ya dolari bilioni 10, au kujenga kituo cha gesi iliyoyeyuka chenye thamani ya dolari bilioni 30, na mradi wa mgodi wa chuma na makaa ya mawe wenye thamani ya dolari bilioni 3.

Katika mazungumzo ya simu kati ya Xi Ping na Samia Hassan mnamo tarehe 22/6/2021, Xi alisema, "China iko tayari kutekeleza mkutano wa Beijing wa Baraza la Ushirikiano kati ya China na Afrika kwa kuzingatia mikakati ya maendeleo ya Tanzania na kupanua ushirikiano katika maeneo kama kilimo, uchukuzi, mawasiliano, utalii na nishati," Samia Hassan alisema, "Tanzania iko tayari kushirikiana na China kuendeleza kikamilifu ujenzi wa pamoja wa Ukanda na Barabara, na itatekeleza kwa dhati matokeo ya Mkutano wa Beijing wa Jukwaa la Ushirikiano wa China na Afrika, na kukuza maendeleo mapya ya uhusiano kati ya China na Afrika. (Uchina CGTN 22/6/2021)

**Tisa:** Kutokana na hili inaeleweka kwamba Uingereza bado inadhibiti kundi la SADC, kwani maamuzi yanafanywa kwa upendeleo wa kuimarisha ushawishi wa Uingereza kwa kuunga mkono tawala zake tanzu. Kutokana na hayo, inaweza kusemwa kwamba Uingereza inaidhibiti Tanzania na vile vile SADC, na kwamba majaribio ya Marekani ya kupenya ndani ya Msumbiji yanasitasita kati ya mafanikio na kushindwa, na hayana utulivu hadi sasa.

Kwa sababu hizi, Tanzania na Msumbiji ni wagombezi wa mzozo wa kimataifa, yaani baina ya Uingereza, ambayo ina ushawishi katika SADC na wanachama wake, na Amerika, ambayo ina nia ya kupanua ushawishi wake mahali pa Uingereza, hasa Msumbiji. Nchi hizi za Kiafrika zitaokolewa tu kutokana na migogoro yake na makucha ya ukoloni kupitia utawala wa Uislamu ambao ni rehma kwa walimwengu wote.

**[وَمَا أَرْسَلْنَاكَ إِلَّا رَحْمَةً لِلْعَالَمِينَ]**

**"Nasi hatukukutuma ila uwe ni Rehema kwa walimwengu wote"** [Al-Anbiya: 107]

**1 Ramadan 1443 H**

**2/4/2022 M**